**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

# TANGAZO LA FURSA KWA VIJANA 5,631 KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KWA KOZI ZA MUDA MFUPI KATIKA VYUO VYA VETA KUPITIA MRADI WA YEFFA

## 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imeingia makubaliano ya ushirikiano na taasisi za AMSHA, RUATI, TAMA na MIBOS kupitia Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakabali wa Chakula na Kilimo (Youth Entrepreneurship for the Future of Food and Agriculture -YEFFA). Mradi huo unafadhiliwa na AGRA Tanzania na unatekelezwa kupitia vyuo vya VETA vya Kihonda, Manyara, Mpanda na Arusha (Oljoro). Mafunzo hayo yanatarajiwa kutolewa kwa awamu nne, ambapo **awamu ya kwanza itaanza tarehe 19 Januari, 2026.**

**Mradi utanufaisha jumla ya vijana wa Kitanzania 5,631** kutoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Lindi, Morogoro, Pwani, Ruvuma, Njombe, Iringa, Manyara, Singida, Dodoma, Tabora, Katavi, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Songwe na Kagera..

VETA inakaribisha maombi ya kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi kupitia mradi wa YEFFA. Mafunzo hayo yatakuwa ni ya kujifunza (kusoma kwa kutwa tu) (Day Programme).

## 2. FANI ZITAKAZOTOLEWA

i) Ufundi wa Zana za Kilimo (Agro-Mechanics)-Muda wa mafunzo wiki nne
ii) Teknolojia ya Umwagiliaji (Irrigation Technology)- Muda wa mafunzo wiki mbili
iii) Teknolojia ya Kuhifadhi Mazao Baada ya Mavuno (Post-Harvest Technology)- Muda wa mafunzo wiki mbili.

## 3. SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

i. Kijana wa Kitanzania mwenye umri kuanzia miaka 15 na 35.
ii. Mwenye mwenye kujua kusoma na kuandika, elimu ya msingi na kuendelea.

## 4. UTARATIBU WA KUOMBA

i. Maombi yatafanyika kwa njia ya mtandao (online application) kupitia mfumo unaopatikana katika tovuti ya VETA: **www.veta.go.tz** au nakala ngumu za fomu (hardcopy) zinazopatikana kwenye vyuo vya VETA Kihonda, Manyara, Mpanda, Moshi, Tanga, Lindi, Pwani, Songea, Iringa, Ludewa, Singida, Dodoma, Tabora, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Kagera na Arusha (Oljoro).
ii. Mwombaji anatakiwa kurejesha fomu akiambatisha cheti cha kuzaliwa au barua ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na vyeti vya elimu aliyonayo.
iii. Fomu zitarejeshwa kwenye chuo husika au kwa njia ya mtandao (online) kupitia mfumo wa maombi.
iv. **Fomu zote zitatolewa bure.**

## 5. KIPINDI CHA MAOMBI

Fomu zitatolewa kuanzia tarehe 19 Desemba, 2025 na mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni tarehe **2 Januari, 2026.**

## 6. ADA NA GHARAMA ZA MAFUNZO

Gharama za ada ya mafunzo pekee zitaalipwa na Mradi. **Gharama nyingine kama nauli, chakula, malazi kwa wanaotoka mbali na vyuo vitakavyotoa mafunzo zitalipwa na mzazi/mlezi/mwanafunzi husika.**

**Wanawake na watu wenye mahitaji maalum watapewa kipaombele.**

Kwa Maelezo na Ufafanuzi zaidi, wasiliana nasi:

VETA Makao Makuu,
12 Barabara ya VETA, 41104 Tambukareli,
S. L. P. 802, Dodoma
Barua pepe: **info@veta.go.tz au pr@veta.go.tz**
Simu ya mkononi: **0755 26 74 89**

**UFUNDI STADI, FURSA KAMA ZOTE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

# FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KATIKA VYUO VYA VETA KIHONDA, MANYARA, MPANDA NA ARUSHA VTC (OLJORO) KUPITIA MRADI WA YEFFA

Bandika picha yako hapa

**FOMU NAMBA: VETA/SC/...... /....../.........**

**A. MAELEZO YA MWOMBAJI (Jaza kwa herufi kubwa)**

1. Jina la Mwombaji ______________________________
(Majina kama yalivyo kwenye vyeti vyako)
2. Jinsi: Me/Ke______________
3. Tarehe ya kuzaliwa ____ /_____ /______ Uraia: ______________________________
4. Namba ya NIDA/Leseni ya gari/Kadi ya mpiga kura ______________________________
5. Kiwango cha Juu cha Elimu yako_____________Mwaka uliohitimu ____________
Ufaulu uliopata_______Jina la shule/chuo ulipohitimu ______________________________
6. Anuani ya Mwombaji: S.L.P ______________________________
Mahali unapoishi: Kijiji/Kata ________________________ Wilaya ____________________
Mkoa_________________Namba ya Simu____________________________
Barua pepe___________________________________________
7. Jina la Mzazi/Mlezi ___________________________________________
Anuani ya Mzazi /Mlezi/Mfadhili S. L. P ______________________________
Namba ya simu___________________________________________
Barua pepe___________________________________________
8. Andika fani unayopenda kujifunza (Majina ya fani ni: 1. Ufundi wa Zana za Kilimo (Agro mechanics) 2. Umwagiliaji (Irrigation) 3. Teknolojia ya Kuhifadhi Mazao Baada ya Mavuno (Post harvest technoology).
i. ______________________________
9. Andika jina la chuo unachopenda kwenda kusoma kuendana na chaguo la fani uliyochagua
a.______________________________

**B. MAELEZO YA YA FOMU.**

(i) Fomu zitaanza kutolewa kuanzia tarehe 19/12/2025 na mwisho wa kuchukua na kurudisha Fomu ni tarehe 02/01/2026

(ii) Matokeo ya waliochaguliwa yatatolewa tarehe 6 January, 2026 na yatabandikwa katika mbao za matangazo chuoni na pia yatawekwa kwenye tovuti ya VETA www.veta.go.tz

**C. MAELEZO MUHIMU**

(i) Weka alama ya vema (√) kwenye aina yeyote ya ulemavu kama unao: Usikivu Hafifu (     ) Uoni Hafifu (     ) Ulemavu wa Ngozi (     ) Ulemavu wa Viungo (     )

(ii) Taja Ulemavu Mwingine kwa kuorodhesha iwapo unao na haujaainishwa katika kipenge (i)________________________________________

**D. UTHIBITISHO**

Nathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa yote yaliyo katika fomu hii, na taarifa nilizotoa ni sahihi.

Saini ya Mwombaji:______________________ Tarehe: ____________________________

Saini ya Mzazi/Mlezi/Mfadhili:________________________________

Tarehe:______________________________